# MWELEKEO WA MSIMU WA MVUA ZA MASIKA (MACHI – MEI), 2025 KWA MKOA WA MJINI MAGHARIBI

**Umetolewa: 23/01/2025**

Taarifa hii inatoa mwelekeo wa msimu wa mvua za Masika katika kipindi cha Machi - Mei, 2025; athari na ushauri kwa sekta mbalimbali katika mkoa wa Mjini Magharibi na wilaya zake:

(I) Ngazi ya Mkoa




Kielelezo 1: (a) Mwelekeo wa msimu wa Masika, 2025 kwa kisiwa cha Unguja . (b) Ramani inayoonesha wastani wa muda mrefu wa mvua za msimu wa Masika katika sehemu mbalimbali za kisiwa cha Unguja. **Angalizo**: Wastani wa muda mrefu (miaka 30) wa mvua za mwezi Machi hadi Mei, mabadiliko ya mvua kati ya mwaka mmoja na mwingine yamezingatiwa.

**Dondoo**

(i) *Kwa ujumla mvua za Wastani hadi Chini ya Wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi ya mkoa wa Mjini Magharibi.*

(ii) *Mvua zinatarajiwa kuanza wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Machi, 2025.*

(iii) *Mvua zinatarajiwa kuisha wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Mei, 2025.*

(iv) *Upo uwezekano wa kutokea vipindi vya ukavu vya siku kumi (10) au zaidi katika msimu huu wa Masika, 2025.*

**Mvua za msimu wa Masika, 2025**

Kwa ujumla mvua zinatarajiwa kuwa za Wastani hadi Chini ya Wastani katika mkoa wa Mjini Magharibi.

***Angalizo:***

*Izingatiwe kuwa matukio ya hali mbaya ya hewa ikiwemo vipindi vya mvua kubwa yanaweza kujitokeza hata katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za Wastani hadi Chini ya Wastani.*

Utabiri wa hali ya hewa nchini na tahadhari zinapatikana katika tovuti ya Mamlaka: **www.meteo.go.tz**

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

(II) Ngazi ya Wilaya

**MWELEKEO WA MVUA ZA MASIKA (MACHI – MEI), 2025 KWA WILAYA YA MJINI**
**Umetolewa: 23/01/2025**

Taarifa hii inatoa mwelekeo wa mvua za Masika katika kipindi cha Machi-Mei, 2025; athari na ushauri kwa Sekta za Kilimo, Mifugo na Uvuvi katika wilaya ya Mjini.




Mwelekeo wa mvua za Masika (Machi-Mei), 2025 kwa wilaya ya Mjini, Unguja.

**Dondoo muhimu**

*(i). Mvua za Wastani hadi Chini ya Wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi ya wilaya ya Mjini.*

*(ii). Mvua zinatarajiwa kuanza wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Machi, 2025.*

*(iii). Mvua zinatarajiwa kuisha wiki ya tatu na ya nne mwezi Mei, 2025.*

*(iv). Wakulima na wafugaji wanashauriwa kutumia mbinu bora za ufugaji na uzalishaji wa mazao ili kukabiliana na upungufu wa mvua.*

## Mvua za msimu wa Masika, 2025 kwa wilaya ya Mjini.

**Zitaanza:** Wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Machi, 2025.

**Zitaisha:** Wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Mei, 2025.

**Kiasi cha mvua zinazotarajiwa:** Mvua zinatarajiwa kuwa za Wastani hadi Chini ya Wastani. Kwa kawaida wastani wa mvua katika miezi ya Machi-Mei kwa wilaya ya Mjini ni kati ya milimita 490 hadi 680.

**Kiwango cha juu cha mvua:** Kinatarajiwa katika mwezi Aprili, 2025.

**Vipindi vya ukavu:** Upo uwezekano wa kutokea vipindi vya ukavu vya siku kumi (10) au zaidi katika msimu huu wa Masika, 2025.

**Ulinganifu:** Mvua zinatarajiwa kuwa chache katika maeneo mengi ukilinganisha na Masika iliyopita.

### Angalizo:

- **Wakulima, wafugaji na wavuvi wanashauriwa kupata ushauri zaidi kutoka kwa maafisa ugani kwa matumizi sahihi ya taarifa za utabiri wa hali ya hewa.**

- **Watumiaji wa taarifa hii wanashauriwa kufuatilia utabiri wa saa 24, siku 10, mwezi pamoja na tahadhari kila zinapotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania.**

## Matokeo na ushauri kwa kilimo, mifugo na uvuvi

### Matokeo

(i) Maeneo ya kutuamisha maji yatapungua na kuruhusu kilimo cha bustani

(ii) Vipindi vya ukavu vinaweza kupelekea kupungua kwa maji na hata kukauka kwa visima, hususan visima vifupi.

(iii) Upungufu wa mvua unaweza kuathiri upatikanaji wa malisho na maji kwa ajili ya mifugo.

### Ushauri

(i) Wakulima wanashauriwa kulima kilimo cha bustani kama vile mbogamboga

(ii) Wananchi wanashauriwa kutumia teknolojia za uvunaji wa maji ya mvua kwa ajili ya matumizi ya baadae

(iii) Mamlaka za maji zinashauriwa kujiandaa na uwezekano wa kutokea kwa upungufu wa maji.

(iv) Wafugaji wa samaki wanashauriwa kuimarisha miundombinu ya ufugaji.

Utabiri wa hali ya hewa nchini na tahadhari zinapatikana katika tovuti ya Mamlaka: **www.meteo.go.tz**

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

**(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)**

727N – 01/2023

(II) Ngazi ya Wilaya

## MWELEKEO WA MVUA ZA MASIKA (MACHI – MEI), 2025 KWA WILAYA YA MAGHARIBI
**Umetolewa: 23/01/2025**

Taarifa hii inatoa mwelekeo wa mvua za Masika katika kipindi cha Machi-Mei, 2025; athari na ushauri kwa Sekta za Kilimo, Mifugo na Uvuvi katika wilaya ya Magharibi.




Mwelekeo wa mvua za Masika (Machi-Mei), 2025 kwa wilaya ya Magharibi, Unguja.

### Dondoo muhimu

*(i).* *Mvua za Wastani hadi Chini ya Wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi ya wilaya ya Magharibi.*

*(ii).* *Mvua zinatarajiwa kuanza wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Machi, 2025.*

*(iii).* *Mvua zinatarajiwa kuisha wiki ya tatu na ya nne mwezi Mei, 2025.*

*(iv).* *Wakulima na wafugaji wanashauriwa kutumia mbinu bora za ufugaji na uzalishaji wa mazao ili kukabiliana na upungufu wa mvua.*

### Mvua za msimu wa Masika, 2025 kwa wilaya ya Magharibi.

**Zitaanza:** Wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Machi, 2025.

**Zitaisha:** Wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Mei, 2025.

**Kiasi cha mvua zinazotarajiwa:** Mvua zinatarajiwa kuwa za Wastani hadi Chini ya Wastani. Kwa kawaida wastani wa mvua katika miezi ya Machi-Mei kwa wilaya ya Magharibi ni kati ya milimita 490 hadi 850.

**Kiwango cha juu cha mvua:** Kinatarajiwa katika mwezi Aprili, 2025.

**Vipindi vya ukavu:** Upo uwezekano wa kutokea vipindi vya ukavu vya siku kumi (10) au zaidi katika msimu huu wa Masika, 2025.

**Ulinganifu:** Mvua zinatarajiwa kuwa chache katika maeneo mengi ukilinganisha na Masika iliyopita.

### Angalizo:

- **Wakulima, wafugaji na wavuvi wanashauriwa kupata ushauri zaidi kutoka kwa maafisa ugani kwa matumizi sahihi ya taarifa za utabiri wa hali ya hewa.**

- **Watumiaji wa taarifa hii wanashauriwa kufuatilia utabiri wa saa 24, siku 10, mwezi pamoja na tahadhari kila zinapotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania.**

### Matokeo na ushauri kwa kilimo, mifugo na uvuvi

#### Matokeo

(i) Upungufu wa unyevunyevu kwenye udongo katika maeneo mengi unaweza kuathiri uzalishaji wa mazao.

(ii) Vipindi vya ukavu vinaweza kupelekea kupungua kwa maji na hata kukauka kwa visima, hususan visima vifupi.

(iii) Upungufu wa mvua unaweza kuathiri upatikanaji wa malisho na maji kwa ajili ya mifugo.

#### Ushauri

(i) Wakulima wanashauriwa kuandaa mashamba, kupanda, kupalilia na kutumia pembejeo husika kwa wakati na kuchagua mbegu na mazao sahihi.

(ii) Wakulima wanashauriwa kutumia mbinu bora za kilimo zinazohifadhi unyevunyevu katika udongo.

(iii) Wafugaji wanashauriwa kutumia mbinu bora za ufugaji ili kutunza malisho na kuvuna maji ya mvua kwa matumizi ya baadae.

(iv) Wafugaji wa samaki wanashauriwa kuimarisha miundombinu ya ufugaji.

Utabiri wa hali ya hewa nchini na tahadhari zinapatikana katika tovuti ya Mamlaka: **www.meteo.go.tz**

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz